**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**Namba za simu**

Mkuu wa shule **0759786526**

Makamu mkuu wa shule **0756426007**

Patron 0752516026

Shule ya sekondari ya Ilongero

S.L.P 972

**Singida**

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi

……………………………………………………………………………………

S.L.P ……………………………….

…………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILONGERO HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA MKOA WA SINGIDA MWAKA …….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha ………. katika shule hii mwaka…………tahasusi ya …………. Shule ya sekondari Ilongero ipo umbali wa Kilometa 22 kaskazini mashariki mwa mji wa Singida. Mwanafunzi akishuka katika **kituo kikuu cha mabasi cha mkoa wa Singida** (Stendi Mpya Misuna) apande bajaji/bodaboda kwa shilingi 1,000/= Kwenda kituo kidogo cha daladala/hiace kiitwacho **Msufini** ambapo mwanafunzi atapata usafiri wa kuja Ilongero kwa nauli ya shilingi **3,000/=,** akifika Ilongero stendi atapanda bajaji/bodaboda kwenda Ilongero Sekondari kwa nauli ya sh 1,000/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe itakayotangazwa na Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

## 1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 1.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili nyeusi mshono wa marinda sio mshono wa jeans, yenye mapana kwa chini inch 17 na shati mbili nyeupe za mikono mirefu
ii. Sare ya Michezo kwa shule hii ni bukta ya blue na fulana ya bluu yenye shingo ya duara ( Babalance) na siyo jezi
iii. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
iv. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
v. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vi. Sweta ya rangi ya bluu shepu ya V shingoni
vii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali za khaki mbili za kitambaa sio mtumba yenye mapana kwa chini inchi 17 na fulana mbili za rangi ya kijani shingo ya duara (Babalance)
viii. Tai mbili nyeusi
ix. Mwanafunzi aje na Tisheti (T-shirt) moja ya shule aina ya form six rangi ya cream. T shirt pia zinapatikana shuleni kwa atakae ikosa madukani

### 1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. counter books kwaya four tano (5), mathematial set, kalamu na penseli
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology, pia inapatikana kwenye duka la shule kwa atakae ikosa madukani
v. Scientific Calculator;
vi. kila mwanafunzi aje na godoro lake lenye saiz 2.5ft x 6ft
vii. Mashuka Jozi 2(rangi ya pinki), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
viii. cheti cha kuhitimu kidato cha nne (result slip) na cheti cha kuzaliwa vyote origina na photocopy zake
ix. Nguo za ndani za kutosha;
x. Vyombo vya chakula ni sahani bati ya mboga tatu kikombe cha bati na kijiko
xi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xii. Galoni moja ya lita 5
xiii. Taulo, ndala, mswaki, dawa ya mswaki, sabuni n.k
xiv. ufagio wa chelewa
xv. Jembe na mpini wake
xvi. Kifaa cha usafi HKL soft broom, HGK ufagio wa kudekia (squizer), HGL reki yenye mpini wa chuma, CBG kwanja, PCM keni ya kumwagilia, PCB hard broom
xvii. sanduku la kutunzia vitu vyake (tranka)
xviii. Mwanafunzi aje na Bima ya afya kwa ajili ya matibabu kama anayo na wale wasio kuanayo waje na **sh 50,400/=** kwaajili ya kuunga nishwa na mfuko wa Bima ya afya NHIF kwa mwaka mmoja

### 1.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MICHANGO HII ILIPWE KUPITIA AKAUNT YA SHULE Na 50801100097 Katika Benki ya NMB jina la akaunti ni ILONGERO SECONDARY SCHOOL tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye risiti ya malipo ya Benk**

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu
vi. yeyote yule;
vii. vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
viii. Kufuga ndevu;
ix. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
x. Uvutaji wa sigara;
xi. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xii. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xiii. Kusababisha mimba;
xiv. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xvi. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvii. Kudharau Bendera ya Taifa;
xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xix. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule MKAKA KAZANA MASYEBA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………...**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0759786526**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0756426007**
- **Mwandamizi Taaluma 0712917739**
- **Mwandamizi Malezi 0752516026**

## KIAMBATISHO A
# HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA

## SHULE YA SEKONDARI ILONGERO

### UTHIBITISHO

**1. Uthibitisho wa Mwanafunzi:**

Mimi ……………………………………………….. nakubali/ sikubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na Kidato cha………. katika shule ya Sekondari Ilongero. Nathibitisha kuwa nitafuata Sheria na Taratibu zote za Shule hii ili nitimize kikamilifu lengo la kuja kwangu hapa kwa manufaa yangu, familia, jamii na Taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na Sheria/Taratibu za Shule nitakubali kuadhibiwa. Naahidi **kutotoroka wala kutochelewa** kurudi shuleni baada ya likizo fupi au ndefu.

Sahihi ya Mwanafunzi………………………………… Tarehe…….……….……………

**2. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:**

Mimi …………………………………………………. nathibitisha kuwa nitatoa gharama zote za Shule pamoja na mahitaji mengine binafsi ya Mwanafunzi kwa lengo la kumuwezesha mwanafunzi huyu asome katika mazingira mazuri kwa kipindi chote atakapokuwa hapo Shuleni kwa kuzingatia Sheria na Taratibu za Shule ya Sekondari Ilongero. Naahidi kwamba mwanangu hatachelewa shuleni kwa kukosa mahitaji (ada, michango n.k)

Saini ya Mzazi/Mlezi ………………………………….. Tarehe ………………………..

**KIAMBATISHO B**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA**
**SHULE YA SEKONDARI ILONGERO**

**1. HISTORIA YA MWANAFUNZI.**

i. Jina la mwanafunzi ……………………… Shule atokayo …………………………

ii. Tarehe ya Kuzaliwa ………………Wilaya aliyozaliwa ……………… Mkoa ……

iii. Dini yako …………………………….. Dhehebu lako ………………………………

iv. Shule ulizosoma kabla ya kuja Ilongero Sekondari:

| S/N | JINA ULILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI/ SEKONDARI | MUDA ULIOSOMA |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |

**2. AFYA:**

i. Taja magojwa yote makubwa uliyowahi kuugua mfano TB, Polio, Kifafa n.k

………………………………………………………………………………………..

ii. Taja matatizo mengine ya Afya yako ……………………………………………..

**3. KUHUSU WAZAZI:**

i. Jina la Mama ………………………………… Hai/ Amefariki lini ………

ii. Jina la Baba ………………………………….. Hai/ Amefariki lini …………

iii. Kazi ya Mama ………………… Dini ………………….. Dhehebu ………

iv. Kazi ya Baba ……………………Dini ………………… Dhehebu …………

v. Anuani ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………..

4. i. Jina la atakaye gharamia mahitaji ya shule ………………………

ii. Kazi yake ni …………………………….. Anuani yake …………………

iii. Uhusiano ………………………… (Mf. Kaka, Dada, Mjomba, Mama, Baba n.k)

vi. Dini yake …………………………………….. Dhehebu …………………

v. Namba za simu za Mzazi/Mlezi ………………………………

Nathibitisha kuwa maelezo yaliyotolewa hapo juu ni sahihi.

Saini ya Mwanafunzi …………..Tarehe …………Saini ya Mzazi/ Mlezi …………..

Tarehe…...

**KIAMBATISHO C**

## SINGIDA DISTRICT COUNCIL
## ILONGERO SECONDARY SCHOOL
### REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A**

To Medial Officer,
………………
………………………

From the Headmaster,
Ilongero Secondary School,
P.O Box 972, **SINGIDA.**

Name: ………………………………………………………

Please examine the above named as to his fitness for a fulltime schooling course.

Date…………………………………  Signature: …………………..

---

**PART B: <u>MEDICAL CERTIFICATE</u>**

(To be completed by Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a fulltime schooling course.

i. a. Eye- sight …………………………  b. Hearing ………………………………...
   c. Limbs ……………………………  d. Speech ………
   e. Leprosy …………………………..  f. Epilepsy …………………
   g. Venereal Diseases ………………………………………

ii. Neuroses ………………………………………………………………………………

iii. Other Serious Diseases …………………………………………

iv. Pregnancy…………………………………

Station…………………………………………………………

Designation: ……………………………Signature and Stamp: ………Date..……….